Ushirika Wa Kindani Na Mungu Aliye Hai

na

Ellis P. Forsman

Ushirika Wa Kindani Na Mungu Aliye Hai

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 8, 2011

Ushirika Wa Kindani Na Mungu Aliye Hai

1 Yohana 1:

Ushirika ni hitaji muhimu kwa mwanadamu. Bila ushirika watu wanateseka; bila ushirika matatizo ya ziada inaongezeka.

Baadhi ya watu hawa fanyi vizuri wanapobaki wenyewe katika ulimwengu.

- Usafi wa kibinafsi unaachwa bila kufanywa.
- Upweke na kukata tama maranyingi vinaingilia.

Rafiki yangu mpendwa alijinyonga baada ya ndugu yake pekee aliyebaki (kaka yake) alipofariki.

Maisha mara nyingi inafurahisha tunaposhirikiana na hao tunao pendana nao.

Gazeti la London lilitoa zawadi ya pesa kwa jibu zuri la swali, "Ni njia ipi iliyofupi kufika London?" Jibu lililoshinda patikana ilikuwa ni " Njia fupi ya kwenda London ni kiwanda kizuri."

Wasafiri wote wanajua nijinsi gani hilo jibu ni la kweli. Kampuni iliyonzuri inafupisha safari yoyote, haijalishi umbali. Katika kampuni kama hiyo muda unaruka, mwendo mrefu, na mwisho unafikiwa karibia kabla mtu hajaligundua.

Safari ya kwenda mbinguni imefupishwa sana, njia imefanywa kuwa rahisi, wakati Yesu Kristo ndiye msafirir mwenzetu.

Ushirika mkuu katika dunia ni ushirika wa Mungu na mwanadamu. Lakin, kwa watu wengi, ushirika huu umeharibiwa kwa sababu ya dhambi zao.

Isa. 59:1-2.*"Tazama mkono wa BWANA si mfupi, isweze kuokoa, au masikio yake ni mazito, asiweze kusikia: lakini makosa yenu yamewatenganisha kati yenu na Mungu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake kwenu, kwamba asiweze kusikia."*

Kila mmoj kwa muda Fulani amewahi kuwa katika hali kama hii na inahitajika ushirika huu uanzishwe au urejezwe.

- Rumi. 3:10, *"Kama ilivyoandikwa, hakuna mwenye haki, hakuna, hata mmoja."*
- Rumi 3:23, "*Kwa maana wote wametenda dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."*

- Rumi. 6:23, *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Yesu Kristo Bwana wetu."*

Kama uhusiano ukiachwa umesimama katika hali kama hii, matokeo ya mwisho ni kukaa milele katika inchi ya moto.

Ushirika wa kindani na Mungu ni muhimu kuwa na uzima wa milele.

Na wakina nani tunaopaswa tuwenao ushirika?

Katika somo hili tunataka kijifunza kuhusu ushirika wa ndani na Mungu aliye hai.

Ushirika na Baba.

1 Yoh. 1:3, *"Hilo tulililoliona na kulisikia, twawahubiri na ninyi; ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi; na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na mwana wake Yesu Kristo."*

Mungu ni muumbaji wetu, Anaye tukinga, Baba, Msaidizi, Mtetezi, Mwenye nguvu, na mwalimu. Hakuna hata moja ya sifa hizi ambazo hatutakiwi kuwa nazo. Lazima tuwe na uthamani wa urafiki kama huo, au tutajikuta sisi wenyewe katika hali mbaya.

Ufu.3:4, *"Lakini unayo majina machache katika Sardi, watu wasitia mavazi yao uchafu. Nao watakwenda pamoja name hali wamevaa mavazi meupe, kwa kuwa wamestahili."*

Wachache katika Sardi walistahili kuwa ushirika wa kindani na Mungu. Kwa nini? Kwa sababu hawakutia mavazi yao uchafu-hawakuishi maisha ya dhambi.

Ushirika na Mwana.

- 1 Wakor. 1:9, *"Mungu ni mwaminifu ambaye mliitwa na yeye mwingie katika ushitika wa Mwanawe, Yesu Kristo Bwana wetu."*
- Math. 18:20, "*Palipo wawili au watatu wamekusanyika kwa jina langu, mimi nipo katikati yao."*
- Yoh. 12:26, *"Mtu akinitumikia na anifuate, nami nilipo ndipo na mtumishi wangu, atakapokuwapo. Tena mtu akinitumikia, Baba atamheshimu."*
- Yoh. 15:15, *"Siwaiti tena watumwa, kwa maana mtumwa hajui atendalo bwana wake; lakini ninyi nimewaita rafiki kwa kuwa yote niliyoyasikia kwa Baba yangu nimewaarifu.*

Yesu aliishi maisha makamilifu bil dhambi kama mfano wetu; Alikufa kifo kibaya msalabani kwa ajili ya dhambi zetu; Alinunua miili yetu kwa damu yake; Alianzisha kanisa ambapo ndugu wanaweza kuja pamoja na kukumbuka dhabihu na kuhimiza kila mmoja; na sasa Anajenga nyumba ya milele kwa ajili ya rafiki zake wapendwa.katika siku ya hukumu ataingilia kati kwa niaba ya watakatifu. Hatuna rafiki mkuu kuliko Yesu. Tunaweza kujaribu kufanya bila urafiki wake?

Ushirika na Roho Mtakatifu.

Wafil. 2:1-2, *"Basi ikiwako faraja yoyote katika Kristo, yakiwako matulizo yoyote ya mapenzi, ukiwako ushirika wowote wa Roho, ikiwako huruma yoyote na rehema, ijalizeni furaha yangu, ili mwe na nia moja, wenye mapenzi mamoja, wenye roho moja, mkinia mamoja."*

Roho Mtakatifu alisaidia kuthibitisha neno katika kipindi cha mitume; Anakaa ndani, na kuwa tia nguvu watoto wa Mungu wapoishi kwa ajili ya Mungu; na anawasaidia Wakristo katika maombi yao kwa Mungu.

- Waru. 8:11-17, *"Lakini ikiwa Roho yake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu. Basi kama ni hivyo, ndugu tu wadeni, si wa mwili tuishi kwa kufuata mambo ya mwili. Kwa maana kama mkiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa, bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi. Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndiyo wana wa Mungu. Kwa kuwa hamkupoe tena roho wa utumwa iletayo hofu, bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani Baba. Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu yakuwa sisi tu watoto wa Mungu, na kama tu watoto basi, tuwarithi; warithi wa Mungu warithio pamoja na Kristo,naam tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye."*
- Waru. 8:26-27, *"Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. Na yeye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo, kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu."*

Kwa msaada huu hatuwezi kufanya kitu bila msada wa Roho Mtakatifu katika maisha yetu. Paulo alikuwa na ushirika wa kindani na Roho Mtakatifu, na akawambia wakristo wawe hivyo ivyo.

Ni nini ushirika wa kindani na Mungu?

Ni nini ambayo siyo.

Siyo ujamaa wa nje — Watu wengi wana dai kuwa “wanamjua Mungu”, lakini wanashindwa kuonyesha kuwa ujamaa kama huo uko katika maisha yao.

Katika hali hiyo naweza nikadai kuwa namfahamu T. A. Willson, mwenyekiti aliyepita wa kampuni ya kutengeneza ndege ya Boeing na sasa anaugonjwa; na Albert Rossellini, gavana wa jimbo la Washington; hawa wote niliwahi kuzungumza nao. Wengi wanadai kuwa ni Wakristo kwa misingi ya kuwa wana Biblia au kwa sababu ndugu zao wanakwenda kanisani. Ushirika wa ndani unahitaji kuonana kila mara.

Ushirika wa ndani na Mungu siyo iliyoegemea katika msingi wako.

Nilipokuwa nafanya kazi katika kiwanda kiitwacho Wind Tunnel tears miaka iliyopita, nilikuwa na uhusiano mzuri na mkuu wangu wa kazi, Jeff. Tulikuwa marafiki, lakini alikuwa na mamlaka. Nilimuheshimu na siku pinga. Aliponipa muongozo, nilifuata kulingana na jinsi alivyotaka ifanyike, siyo jinsi ninavyofikiria. Wakati Jeff alipokuwa akitoka, wakati mwingine alimuweka katika uongozi. Hakuna kati yetu aliyepewa majukumu ya mamlaka lakini tulikuwa tunafanya kulingana na tulivyopewa maagizo. Unafikiria nini ambacho kingekuwa matokeo kama nikimwambia Jeff (au Mark kama angekuwa katika mamlaka), “sitafanya hilo!”? Nitajikuta mwenyewe nikiharibu uhusiano, tukiwa tumeadhibiwa, na ikiwezekana kufukuzwa kabisa kwa sababu ya nidhamu ya kuchukulia kwa mzaha mamlaka yao.

Watu wengi leo hawafahamu kuwa wanaharibu uhusiano wao na Mungu na wakiacha mamlaka yake wanapokataa mwongozo wake. Wanafanya hivi wanapo toa kauli hii, “sidhani kama ubatizo ni muhimu”, au “kanisa Lolote” au “wanafurahisha” badala ya kuhubiri neno la Mungu.

Waru. 1:16-17, *“Kwa maana siionei haya injili ya Kristo: kwa maana ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na pia kwa Muyunani. Kwa maana haki ya Mungu imefunuliwa ktoka imani hadi imani: kama ilivyoandikwa, mwenye haki ataishi kwa imani.”*

Ushirika wa ndani na Mungu ni zaidi ya uhusiano wa ziada (kama huduma ya kwanza).

Kwa watu wengine wanakuwa katika hali ya kutishiwa maisha kabla hawaja mfikiria Mungu.

Ushirikiano na Mungu ni.

Kujitoa mathubuti.

Math. 16:24, *"Yesu akawambia wanafunzi wake, yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, achukuwe msalaba wake anifuate."*

Kubeba msalaba siyokukaa na njaa, magonjwa, hali mbaya ya hewa, au chochote katika maisha ambayo haipo sahihi, bali ni kukubali mzigo wa maisha kwa ajili ya mapenzi ya Mungu. Kama ilivyokweli mkristo anapojikana mwenyewe raha ya maisha haya, kubeba msalaba inamaanisha kujikana kikamilifu na dhihaka yaw engine tunapo simama upande wa Mungu katika maisha yetu.

Ushirika wa ndani na Mungu ni moja iliyo katika msingi wake.

Yoh.14:6, *"Yesu akamwambia, mimi ni njia, kweli na uzima, mtu haji kwa Baba, ila kwa mimi.*

Watu wengi wanapenda kusikiliza yohana 15:16 na kuwaambia watu wengine maneno yake.

Yoh.15:16, "*Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda, na matunda yenu yapate kukaa, ili kwamba lolote mmwombalo Baba kwa jina langu awapeni.*"

Wana sisitiza *"vyovyote"* tunaomba tutapata, lakini wanakataa nyingine "*vyovyote"* misitari miwili tu inayoendelea mbele yah ii misitari:

Yoh. 15:14, *"Ninyi ni marafiki zangu,* ***kama*** *mkifanya niwaamuruyo"*

Upendo wa Mungu **ni** wa masharti. Yeye ndiye aliyeweka neno, *"kama"* katika uhusiano wetu. Isipokuwa tukiwa marafiki zake hali ya maombi yetu haiwezi kusikika. Nimewahi kusikia muinjilisti katika redio akidai kwamba Kristo hakuweka upendo wa masharti. Kwakweli hajui anachokiongea.

- Yoh. 15:14, *"Ninyi ni rafiki zangu,* **kama** mkifanya niwaamuruyo."
- Yoh. 14:15**, *"Kama*** *mkinipenda mtazishika amri zangu."*

Ushirika wa kindani na Mungu mhimili wake hutoka katika upendo.

1 Yoh. 4:19, "*Tunampenda, kwa sababu alitupenda kwanza."*

Yesu ameosha upendo wake kwetu kwa kutoa uhai wake msalabani. Upendo wake ulimsababisha afanye tendo. Yohana15:13, "*Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake.*"

Marafiki zake pia wanatoa upendo wao kwake. Waef.6:24, "*Neema na iwe pamoja na wote wampendao Bwana wetu Yesu Kristo katika hali ya kutokuharibika.*"

Upendo huo lazima uwe upendo wa kweli- ambaye hachakai tunapo jisikia kwamba Yesu haitajiki; upendo uliyo kamili katika wakati wetu mzuri sawasawa na ubaya wetu. Tunapo muonyesha kuwa tuna mpenda, atakaa katikati yetu.

1 Yoh. 4:16, "*Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi, na kuamini. Mungu ni pendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu na Mungu hukaa ndani yake.*"

Tukimpenda matendo yetu yataonyesha.

Kinyume (kinyume): ukikataa kuishi kwa Mungu, usimtarajie kukaa ndani yako, kwa sababu hawezi.

Jinsi baadhi walivyo jitoa

Wenye moyo nusu.

Kama mke wa Lutu. Alijiingiza katika majaribu akaangalia nyuma kuwaona marafiki zake na ndugu zake waliobaki nyuma wakati Mungu alipoangamiza miji ya Sodoma, baada ya Mungu kusema wasiangalie nyuma.

Luka 17:31-32, *"katika siku ile aliye juu ya dari, na vyombo vyake vimo ndani ya nyumba, asishuke ili kuvitwaa; kadhalika aliyeshambani asirejee nyuma. Mkumbukeni mkewe Lutu."*

Alifanya kitendo kinyume na kile ambacho Mungu alitaka lifanyike.

Tukichukua huduma ya Mungu katika maisha yetu, tusiwe na hamu ya kuangalia nyuma katika maisha yetu yaliyopita. Tunapokuwa Wakristo mtazamo wetu ni kuwa katika Yesu Kristo na huduma yetu kwake.

2 Petr. 2:20-22, *"Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza. Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kuijua kasha kuiacha ile amri takatifu waliopewa. Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, mbwa amerudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaagaa matopeni."*

Hebu na tusimtumikie kwa moyo nusu. Mungu hamuangalii Mkristo mwenye uvuguvugu.

Wanaosita (Wanao kalifu).

Watuwengi wanasita na huduma yao kwa Mungu. Wamezidiwa na kujali maisha ya ulimwengu huu.

Luka 8:11-14, *"Na huo mfano maana yake ni hii; mbegu ni neno la Mungu. Wale wa karibu na nji ndio wasikiao, kasha huja ibilisi akaliondoa hilo neno mioyoni mwao, wasije wakaamini na kuokoka. Na wale penye mwamba ndio wale ambao wasikiapo hulipokea lile neno kwa furaha; nao hawana mizizi, huamini kitambo kidogo, na wakati wa kujaribiwa kujitenga. Na zilizoanguka penye miiba ni wale waliosikia na katika kuenenda kwao husongwa na shughuli na mali, na anasa za maisha haya, wasiivishe lolote."*

Tunaporuhusu maisha ya dunia hii yachukue nafasi katika maisha yetu, upendo wetu kwa Yesu Kristo hautakuwa na nguvu ya kutosha ili kutukidhi. Tukimweka wa kwanza katika maisha yetu, atajali mahitaji yetu.

Hii inajumlisha kazi zetu, shule, michezo, nk. Tukiruhusu yaingilie uhusiano wetu na yeye.

Kwa Udhuru.

Baadhi ya watu hutoa udhuru.

Luka 14:16-24, *"Akamwambia mtu mmoja alifanya karamu kubwa, akaalika watu wengi, akamtuma mtumwa wake saa ya chakula awaambie wale walioalikwa, njooni kwakuwa vitu vyote vimekwisha kuwekwa tayari. Wakaanza wote kutoa udhuru kwa nia moja. Wa kwanza alimwambia, nimenunua shamba, sharti niende nikalitazame; tafadhali unisamehe. Mwingine akasema nimenuna ng'ombe jozi tano, nina kwenda kuwa jaribu, tafadhali unisamehe. Mwingine akasema nimeoa mke na kwa sababu hiyo siwezi kuja. Yule mtumwa akaenda akampa bwana wake habari ya mambo hayo. Basi Yule mwenye nyumba akakasirika, akamwambia mtumwa wake, toka upesi uende katika njia kuu na vichochoro vya mji ukawalete hapa maskini, na vilema, na vipofu na viwete. Mtumwa aksema, Bwana, hayo ulioagiza yamekwisha tendeka, na hata sasa ingaliko nafasi. Bwana akamwambia mtumwa, toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani nyumba yangu ipate kujaa. Maana nawambia ya kwamba katika wale walioalikwa, hapana hata mmoja atakayeionja karamu yangu."*

Ushirika na Mungu inahitaji kujitoa kikwelikweli, siyo mtu anaye tafuta sababu.

Ushirika wa kindani na Mungu unaanzaje?

Katika kutambua dhambi.

Tunapaswa kutambua kuwa tunapofanya dhambi ushirika wetu na Mungu ikohatarini. Tunapogundua kwamba hali hii imetokea, tunatakiwa tu tubu na kutii injili.

Wakati tanakimbia machafuko ya ulimwengu, tunaweza kuwa washirika wa upendo wa Mungu na ahadi zake.

Wengine wanafiria dhambi zao zimekuwa kubwa kiasi kwamba hawawezi kufikiria kuhusu kuwa wakristo. Paulo ni mfano wa mtu aliyekuwa gizani, lakini alibadilika. Petro alimkana Kristo, lakini alitubu. Kumbuka kila mmoja ametenda dhambi. Haukopeke yako. Unaweza ukazikimbia dhambi zako!

2 Petr. 1:4, *"Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tama."*

Kwa, hiyo dhambi lazima ife katika maisha yetu ili tufurahie ushirika wetu na Mungu.

Waru. 6:1-6, *"Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike tusitumikie dhambi tena."*

Kama tukikataa dhambi katika maisha yetu na kuukubali ushirika wa Yesu, maisha yetu yatakuwa na utajiri mwingi.

Ua la dhalili lililobaki lenyewe itabaki dhalili. Miongoni mwa Wadachi ua muda Fulani ililimwa kwa kupandikiza ua la dhalili karibu kabisa na ua lililo na dhamani. Ua la dhalili ubora wake ulitazamwa kwa makini, na mwana ndani ilitolewa ili kuzuia kujikuza yenyewe; lengo likiwa ni kwamba isije ikaambukizwa na ua bora.

Hivi ndivyo maisha yetu yanapaswa kuwa sawa na ile ya Yesu. Kama maisha yetu yakichafuliwa kama zamani, na haki yake katika mioyo yetu, hivyo tutakosa udhamani wetu, na kubadilishwa katika ubora zaidi ndani ya Kristo.

Maisha yetu lazima yamlikwe na mwenendo mtakatifu kama sivyo maisha yetu ni ya uongo. Baadhi wana kwenda kanisani juma pili, lakini katikati ya wiki wanaishi maisha kanakwamba Mungu hayupo.

1 Yoh. 1:6-7, "*Tukisema ya kwamba twashirikiana naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli. Bali tukienenda nuruni kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana* sisi *kwa sisi na damu yake Yesu Mwana wake yatusafisha dhambi yote."*

Waenda kanisani wenzako wakikuona unaishi maisha ya ulimwengu, ushirika wako na wao unazuiwa.

Ni matokeo yapi yanayotoke katika ushurika wa kindani na Mungu?

Ushirika.

Na Mungu, Kristo, Roho Mtakatifu. (angalia 1 Yoh.1:6-7 hapo juu). Sisi kwa sisi. (angalia 1 Yoh 1:6-7).

Matokeo ya ushirika wa ndani na Mungu yameonyeshwa katika masha yetu na matendo. Tunaonyesha upendo, uvumilivu, furaha, amani, nk. Katika maisha yetu.

Tuna ushirika wa ndani na injili.

Wafil. 1:3-5, "*Namshukuru Mungu wangu kila niwakumbukapo, sikuzote kila niwaombeapo ninyi nyote nikisema sala zangu kwa furaha, kwa sababu ya ushirika wenu katika kuieneza injili tangu siku ile ya kwanza hata leo hivi."*

Tukimpenda Mungu kiukweli, hamyetu lazima iwe katika maneno yake aliyotupatia.

Nasikia watu husema kuwa kanisa linachosha; kusoma Biblia inachosha. Hapa kuna hadithi kuhusu binti na mwandishi:

Binti huyu aliweka kitabu chini mbayo alimaliza muda mfupi, kwa lengo kwa ilikuwa ni kitabu kibaya ambacho hajawahi kusoma

Kwa sababu ya muda, alikutana na kijana mmoja; na usiku mmoja akamwambia, "nina kitabu katika maktaba yangu ambayo jina la mwandishi wake, na pia matendo yanaendana na yako. Unadhani hilo ni tukio geni?"

"Sidhani" mvulan alijibu.

"Kwa nini?", msichana akasema.

"Kwa sababu rahisi, kwamba niliandika kitabu."

Usiku huo binti huyu alisimama hadi saa 8 asubuhi akisoma kitabu tena. Na wakati huu ilionekana kuwa ni kitabu kilichovutia sana.

Kitabu ambacho kilikuwa kibaya sasa kilivutia kwa sababu alijua na kumpenda mwandishi.

Hivyo, mwana wa Mungu anapoona Biblia inavutia ni kwa sababu anajua na anampenda mwandishi!

Kama tukifikiria kuwa Biblia ni mbaya, ni muda wa kuangalia uhusiano wetu na Mungu.

Hitimisho

Vipi kuhusu wewe? Je upo katika ushirika na Mungu? Ushirika huo ni wa kindani kiasi gani?

Kama kunakitu katika maisha yako ambayo ina sababisha dosari katika ushirika huo na Mungu, kwa nini usikifanyie kitu leo?

Usiwe kama Felix, aliyemwambia Paulo, *"nenda njia yako kwa sasa; nikiwa na muda mwafaka, nitakuita."* Haijaonyesha kwamba huu "muda mwafaka" aliupata.

Kwa nini usibadilishe uhusiano wako na Mungu leo? Kwa nini usiwe na uhusiano wa kindani naye?